

102/3
KISWAHILI
FASIHI
KARATASI 3
MEI / JUNI, 2014

MUDA: SAA 2 ½

MTIHANI WA BUNYORE – MARANDA (BUMA II)
MTIHANI TANGULIZI MWIGO (KIMWIGO)

MAAGIZO

- a) Jibu maswali manne pekee
- b) Swali la kwanza ni lazima
- c) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki, yaani:
Riwaya, Tamthilia, Hadithi Fupi na Fasihi Simulizi
- d) Usijibu maswali mawili kutoka sehemuy moja
- e) Karatasi hii ina kurasa 4 zilizopigwa chapa
- f) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kuwa maswali yote yamo na kuwa kurasa zote zimepigwa chapa sawasawa.
- g) Kumbuka kuchora jedwali la maswali uliyoyajibu juu ya karatasi yako ya majibu

SEHEMU A: USHAIRI (alama 20)

1. (LAZIMA)

Siafu Wamekazana

Nyoka amegutuka, ndani ya shimo kutuna,
Tena amekasirika, hasira zenye kununa,
Nyoka anababaika, shimoni kwa kujikuna,
Siafu wamekazana, nyoka amekasirika.

Shimoni ataondoka, hilo nataja kwa jina,
Nyoka anajuwa fika, siafu wakiungana,
Nguvu zao zongezeka, shimoni watagomana,
Siafu wamekazana, nyoka amekasirika.

Siafu wakijishika, mshiko kushikamana,
Kwamba wanampeleka, sultani wao bwana,
Shimoni wanapofika, nyoka la kufanya hana,
Siafu wamekazana, nyoka amekasirika.

Siafu wanapofika, na nyoka wakikutana,
Nyoka hawezi kufoka, huwa ametulizana,
Ndipo nyoka huondoka, na wana wakilizana,
Siafu wamekazana, nyoka amekasirika.

Kupo na kukanganyika, hilo na natujue sana,
Nyoka anapoondoka, siafu hulaliana,
Huuma hupumzika, hapo hakutafanana,
Siafu wamekazana, nyoka amekasirika.

Nyoka akishaondoka, na siafu hujazana,
Shimoni wakipeleka, vyakula kutiliana,
Ndilo walilotaka, wale kwa kutulizana
Siafu wamekazana, nyoka amekasirika.

(S. Abdu Kandoro)

Maswali

- a) Shairi hili linazungumzia nini? (alama 2)
- b) Ukitumia vigezo vifuatavyo, eleza aina za shairi hili. (alama 2)
- I. Vipande
- II. Vina
- c) Baninisha matumizi manne ya Jazanda katika utungo huu. (alama 4)

- d) Andika ubeti wa sita kwa lugha nathari (alama 4)
- e) Onyesha mtunzi alivyotumia kibali chake cha utunzi katika ubeti wa pili. (alama 4)
- f) Fafanua umuhimu wa mkarara wa shairi hili. (alama 4)

SEHEMU B: RIWAYA

Ken Walibora: Kidagaa Kimemwozea

Jibu swali la 2 au la 3

2. “Kahakikisha kwamba lengo lao moja nalo ni kumnyonya kipugnug”
- a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- b) Fafanua namna kipungu alivyonyonyolewa (alama 10)
- c) Eleza umuhimu sita wa mhusika anayerejelewa kama kupungu. (alama 6)
3. Jadili mchango wa wahusika Imani na Amani katika ujenzi wa jamii mpya. (alama 20)

SEHEMU C: TAMTHILIA

T.M. Arege: Mstahiki Meya

Jibu swali la 4 au la 5

4. “Uvundo haswa! Hata hao wageni sijui wataonaje hali hii. aibu kubwa inatungoja kama watakuja.”
- a. Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- b. Kwa kutolea mifano taja mbinu mbili za utunzi zinazojitokeza katika dondoo hili (alama 4)
- c. Eleza uvundo unaorejelewa kaitika baraza la mji wa Cheneo kwa jumla (alama 12)
5. “Ukoloni mamboleo ni kizingiti kikuu dhidi ya ustawi katika mataifa mengi barani Afrika. Thibitisha. (alama 20)

SEHEMU D: HADITHI FUPI NA FASIHI SIMULIZI

Jibu swali la 6 au 7

HADITHI FUPI

Ken Walibora na S. M. Mohamed: Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine.

6. “Mimi nani? Mja nisiye na shukrani. Nisiyefadhilika au nisiyehisi. Mja wa laana, mbwa miye, mi..mi..mi..e.”
- a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- b) Taja na utoe mfano wa mbinu mbili za fasihi zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 4)
- c) Eleza hali ya mzungumzaji kama inavyodhihirika katika dondoo hili. (alama 2)
- d) “Ulevi una madhara chungu nzima katika jamii.” Thibitisha kwa kurejelea hadithi husika. (alama 10)

FASIHI SIMULIZI

7. a) Tofautisha na ulinganihse mighan na maghani (alama 4)
- b) Huku ukitolea mifano ya kiperu husika, fafania dhima nne za maghani. (alama 8)
- c) Ukifuata utratibu unaokubalika, onyesha hatua sita za uwasilishaji wa vitendawili. (alama 6)